



# JIVI LETU, MAZINGIRA YETU, KESHO YETU:

## Thamani ya uoto wa asili ndani ya Jiji la Dar es salaam

Tanzania ni nchi yenye utajiri mkubwa na wa kipekee wa bayoanuai, milima inayozunguka upande wa Mashariki mwa nchi na misitu ya pwani inafanya nchi iwe ni moja kati ya nchi 25 duniani zenye vitovu vya bayoanuai. Hata kama jiji linakua kwa kasi, Dar es salaam bado imekuwa na maeneo mengi ya asili ambayo yana faida na yanatoa huduma muhimu kwenye jiji na watu wake: Pwani nzuri na fukwe zenye mandhari nzuri, mito na vijito, mikoko, misitu na aina mbali mbali za wanyama pori.

Kwa mipango thabiti, rasilimali hizi za asili zinatakiwa zilindwe, zitunzwe, zirejeshwe, zikuzwe na hata kuongezwa ili kuendelea kutoa faida. Faida hizo ni maji safi, chakula, ajira, kuratibu hali joto la jiji, kupunguza uchafuzi wa hali ya hewa, kutukinga na majanga ya asili, fursa za utalii, maeneo ya starehe na mapumziko na kujisikia fahari juu ya maeneo yetu.

### Dar es Salaam: Faida za uoto wa asili na athari zake

Kundi la mali asilia	Faida za uoto wa asili	Athari za ukosefu wa uoto wa asili
<b>Maeneo Kijani Ya wazi</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kuratibu joto la jiji</li> <li>Kupunguza athari za mafuriko</li> <li>Kuzuia Uchafuzi wa mazingira</li> <li>Mapumziko na kustarehe</li> <li>Makazi ya maisha ya wanyama pori (Plants and animals)</li> <li>Utunzaji wa wa Bayoanuai</li> <li>Kujifunza na Elimu</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Jiji kukua na uwepo wa makazi holela</li> <li>Ukosefu wa maboresho ya maeneo ya wazi</li> <li>Kutokuwepo kwa furaha na kujali mazingira</li> <li>Uvamizi wa viembe wageni (aliens species) kama kunguru nk</li> </ul>
<b>Mito na ardhi Oevu</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Vyanzo vya maji kwa matumizi ya nyumbani na kilimo</li> <li>Kusafisha maji</li> <li>Kustarehe</li> <li>Usafi</li> <li>Kuzuia Mafuriko</li> <li>Kutunza Bayoanuai na mwonekano wa ardhi</li> <li>Kupunguza Joto</li> <li>Kuongeza maji ya chini ya ardhi</li> <li>Uhifadhi wa virutubisho ardhi</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Uchafuzi wa mazingira na udhibiti mbovu wa taka (taka maji na taka ngumu)</li> <li>Kujanga makazi ndani na karibu na misaka ya mito</li> <li>Mitaro na taka kutoka viwandani hutiririsha maji machafu na utupaji ovyo wa taka</li> <li>Uchimbaji wa mchanga</li> <li>Kutoweka kwa misitu</li> </ul>
<b>Mazingira ya baharini</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Shehena ya samaki, ajira za ndani na maisha ya watu</li> <li>Matumbawe kuzaliana, miche, malisho na sehemu ya makazi kwa wanyama kama samaki, kaa na aina nyingine ambayo inasaidia kwenye uvuvi</li> <li>Matumbawe yanatengeneza uzio asilia kwa kulinda pwani isiharibiwe na mawimbi na vimbunga</li> <li>Bahari ni mahali pa kufyonza hewa ya kaboni</li> <li>Fursa za kiutalii</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Uvuvi uliozidi kipimo</li> <li>Matumizi ya zana harifu katika shughuli za uvuvi</li> <li>Mito iliyoachafuwa kutiririsha maji baharini na kuathiri maisha ya viembe hai wa baharini</li> <li>Ukosefu wa kanuni</li> <li>Kuathiriwa kwa shughuli za utalii</li> </ul>
<b>Pwani: Fukwe na maeneo ya bahari</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Utalii</li> <li>Maeneo ya starehe</li> <li>Makazi na chakula (seagrass) kwa viembe hai walio hatarini kutoweka kama kasa, nyangumi, humpback na papa nyangumi</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Uchafuzi (utupaji wa taka ovyo, taka ngumu, uchafuzi wa viwanda na taka) maeneo ya fukwe</li> <li>Uharibu wa ardhi na mfumo wa viembe hai baharini umepotekea kuwepo kwa mchanga na mawimbi makali kwenye maeneo ya pwani</li> </ul>
<b>Misitu ya Pwani na Mpori</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Mimea ya madawa, kuni, malighafi za ujenji na chakula</li> <li>Utunzaji wa sehemu za juu za mto, vyanzo vya mito na sehemu za mito inapogawanyika</li> <li>Kuratibu joto la jiji</li> <li>Maeneo ya kustarehe</li> <li>Utalii</li> <li>Kusaidia kuwepo makazi ya wanyama pori (mimea na wanyama)</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Matumizi yasiyo endelevu kwenye rasimili misitu</li> <li>Uchomaji wa mkaa holela, ufugaji wa mifugo holela, kuchoma moto, na uvunaji wa kuni holela, uwindaji, ujangili na utinaji asili na shughuli za ujenji</li> </ul>
<b>Mikoko</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Uwepo wa vitaru vya uzalishaji wa sama ki na samaki Kamba</li> <li>Kujikinga na mmomonyoko wa udongo na kuongezeka kwa kiwango cha maji ya bahari</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kubadilisha sehemu ya mikoko kuwa majaruba ya kilimo cha mpunga, uvunaji wa chumvi, kilimo cha samaki na ukauji wa jiji</li> <li>Taka, mafuta na uchafuzi wa viwanda usioratibiwa na kutiririshwa kwa maji machafu kwenye mito</li> <li>Mchanga unaotokana na mmomonyoko na madawa ya mimea kutiririka mitoni</li> <li>Uvunaji usioendelevu wa miti ya mikoko kwa ajili ya mbao za ujenji</li> <li>Uvunaji miti uliozidi kiasi kwa ajili ya kuni na ukaushaji wa samaki</li> </ul>

Shukrani: Kamati ya kuratibu Muungiliano wa Bayoanuai Dar es salaam na wataalam wa ndani wa bayoanuai kama ilivyo orodheshwa kwenye mpangilio wa kitabu cha ramani ya Dar es salaam 2018.

Kuelekea Morogoro na Dodoma

## Dar es Salaam, Tanzania

Idadi ya Watu: 4.4 million Kiwango cha Ongezeko la Watu: Asilimia 6.5 Eneo: Kilomita za Mraba 1630

Mchoro huu, ulichorwa kwa kuunganisha takwimu mpya za ardhi kijiografia, maarifa ya wataalam wa ndani na maandiko ya hivi karibuni na nchi kuhusu uoto wa asili katika jiji la Dar es salaam. Lengoni ni kutoa taswira ya kuvutia kuhusu mwonekano wa uoto wa asili katika jiji la Dar es salaam.

Kuelekea Mtwara na Msumbiji

